

SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

E-mail : <blm@zanlink.com>
Nambari ya Sim : 2231823

BARAZA LA MAPINDUZI
S. L. P 437
ZANZIBAR - TANZANIA.

Kumb. Nam. BLM/98/U.M/C.4/VOL.1/60 Tarehe 11 JANUARI, 2011

MAKATIBU WAKUU,
SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR.


YAH: AJIRA ZA MKATABA KATIKA NGAZI ZA UTEUZI WA MHESHIMIWA RAIS

Kwa heshima naomba kukuarifuni kwamba watu wote wanaojiriwa kwa mikataba na ambao wapo katika ngazi za uteuzi wa Mheshimiwa Rais hawatahusika na utaratibu wa kulipwa mshahara ambao tayari umejumuishwa posho mbali mbali yaani "consolidation salaries" na badala yake watalipwa mshahara (usiojumuishwa posho), na watalipwa posho nyengine wanazostahiki kutokana na wadhifa walioteuliwa.

Pamoja na barua hii nakuleteeni na kiambatisho ambacho kinaonesha kiwango cha mshahara na posho mbali mbali kwa watu wataojiriwa kwa mikataba kwa ngazi za uteuzi wa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Mshahara na posho kwa wateuliwa wa Mhe. Rais wataojiriwa kwa mikataba na ambao vya vyao haviwiani kimaslahi na nyadhifa zilizotajwa katika kiambatisho itapangwa na kutolewa ufafanuzi na Ofisi ya Rais, (Utumishi wa Umma na Utawala Bora).

Mikataba yote ambayo imetiwa saina kabla ya kutolewa ufafanuzi huu irekebishwe ipasavyo.

Wako Mtiifu,


(DK. ABDULHAMID Y. MZEE)
KATIBU WA BARAZA LA MAPINDUZI
NA KATIBU MKUU KIONGOZI,
ZANZIBAR.

Noida:

Mwenyekiti, Tume ya Utumishi Serikalini.
Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais (Utumishi wa Umma na Utawala wa Bora).
Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais (Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo).
Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.
Mkasibu Mkuu wa Serikali,



**MISHAHARA NA POSHO KWA AJILI YA VIONGOZI WATENDAJI WALIOMO
KATIKA UTEUZI WA MHESHIMIWA RAIS AMBAO WATAAJIRIWA KWA MKATABA:**

WADHIFA	MSHAHARA	POSHO MBALI MBALI					WATUMISHI
		MAFUTA	TAKRIMA	UMEME	SIMU	NYUMBA*	
Katibu Mkuu au Wadhifa Mwingine Unaowiana Kimaslahi	530,000/=	992,000/=	20,000/=	82,600/=	120,000/=	265,000/=	200,000/=
Naibu Katibu Mkuu au Wadhifa Mwingine Unaowiana Kimaslahi	480,000/=	992,000/=	20,000/=	82,600/=	120,000/=	240,000/=	200,000/=
Kamishna au Wadhifa Mwingine Unaowiana Kimaslahi	430,000/=	744,000/=	15,000/=	68,440/=	75,000/=	215,000/=	-
Mkurugenzi/Afisa Mdamini au Wadhifa Mwingine Unaowiana Kimaslahi	380,000/=	744,000/=	10,000/=	54,280/=	50,000/=	190,000/=	-
Naibu Mkurugenzi au Wadhifa Mwingine Unaowiana Kimaslahi	330,000/=	744,000/=	10,000/=	54,280/=	50,000/=	165,000/=	-

* Mtendaji ataeishi katika nyumba ya Serikali atapaswa kulipa kodi ya nyumba.